

IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

1.0 UTANGULIZI

Idara ya Mifugo na Uvuvu ina jukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvu katika Halmashauri.

1.1 WATUMISHI

Idara ya Mifugo na Uvuvu ina jumla ya watumishi 10 kati ya hao watumishi 8 ni wa Mifugo na watumishi 2 ni wa Uvuvu kama mchanganuo unavyoonesha katika jedwali hapa chini:

KITENGO	OFISI KUU	KATA/VIJIJI
Mifugo	3	5
Uvuvu	1	1
JUMLA	4	6



Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvu Ndugu Elia Shemtoi (asiyevaa Koti) akitoa maelekezo kwa Wanafunzi wa Chuo cha

Kilimo KATRIN kabla ya kuanza zoezi la chanjo dhidi ya Kichaa cha Mbwa

1.2. SEKTA YA MIFUGO

Sekta ya Mifugo inatekeleza shughuli kwa mujibu wa muundo usuatao

Huduma za Mifugo (Veterinary Services) .

Kuratibu na kusimamia udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

Kusimamia utoaji wa huduma za afya ya wanyama pamoja na kuwawezesha watoa huduma za afya ya wanyama katika kutoa huduma kama vile Tiba na Chanjo kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni

Kusimamia ukaguzi wa nyama na usafi wa machinjio.

Kusimamia na kudhibiti uingizaji na utoaji wa wanyama na mazao yake ndani ya Halmashauri.

Kusimamia utoaji wa huduma za afya ya wanyama pamoja na kuwawezesha watoa huduma za afya ya wanyama katika kutoa huduma kama vile Tiba na Chanjo kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni.

Kupanga program za muda mfupi, wa kati na mrefu katika kudhibiti magonjwa ya wanyama.
Kusimamia uingizaji na usambazaji wa pembejeo za Mifugo.
Kukusanya na kuchambua taarifa za magonjwa ya wanyama kwa ajili ya matumizi mbalimbali.
Kusimamia utekelezaji wa sheria za Magonjwa ya Wanyama, sheria ya Veternari na kanuni zake na
Sheria ndogo za Mifugo



Wataalam wa Mifugo wakiendesha zoezi la Chanjo dhidi ya Kichaa cha Mbwa katika Halmashauri ya Mji Ifakara

Huduma za Ugani (Livestock Extension Services)

Kusimamia uendeshaji wa shughuli za huduma za ugani katika Halmashauri.

Kuandaa orodha ya watoa huduma binafsi zikiwemo NGO's na kuwawezesha kutoa huduma za ugani.

Kukusanya na kuchambua takwimu za Mifugo katika ngazi za kata na Halmashauri.

Kuwasaidia maafisa ugani kufanya kazi na vikundi vya wafugaji ili waweze kufikia malengo.

Kuandaa vifaa vya kufundishia wafugaji kama vitini, mabango, vijitabu vidogo na machapisho muhimu kwa ajili ya kutolewa huduma za ugani.

Kiunganishi kati ya watafiti, maafisa ugani, wafugaji na vikundi vya wafugaji katika programu mbalimbali zinazohusu sekta ya Mifugo.

Kuratibu na kusimamia uhusiano na vikundi vya wafugaji , NGO'S na watoa huduma za Mifugo katika Halmashauri.





Machinjio ya Kisasa iliyopo Kapolo ikiendelea na Ujenzi

Usimamizi wa nyama na ngozi (Meat, Hides and Skins)

Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Nyama na Kanuni zake.

Kuwawezesha sekta binafsi kuwekeza kibashara katika sekta ndogo ya nyama na ngozi.

Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi na uhifadhi wa ngozi (Hides and Skin).

Kuangalia uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na mfumo wa masoko wa ngozi (Hides and Skin).

Kupitia mara kwa mara mfumo wa masoko wa nyama na ngozi katika Halmashauri





Uzalishaji na ukaguzi wa maziwa (Dairy)

Kuwahamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ndogo ya maziwa (uzalishaji na usindikaji), kuwahamasisha kuunda vikundi vya ukusanyaji, upoozaji na uuzaji wa maziwa.

Kuratibu na kuhimiza uboreshaji wa kosaifu kwa ng'ombe wa maziwa na wa asili kwa mujibu wa Sera ya Taifa.

Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maziwa na Kanuni zake.

Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa Mifugo (Livestock identification ,Registration and Traceability)

Kuandaa na kusimamia ukusanyaji wa takwimu za Mifugo

Kutambua na kusajili mifugo yote iliyopo katika Halmashauri

Kusimamia sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo

Uzalishaji wa wanyama wadogo (Small Stocks)

Kuandaa mipango ya uboreshaji wa wanyama wadogo

Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji na masoko ya wanyama wadogo pamoja na mazao yao

Kupitia mara kwa mara mfumo wa masoko wa wanyama wadogo ndani na nje ya Halmashauri

Mifumo ya ufugaji

Kuelimisha wafugaji juu ya matumizi sahihi ya nyanda za malisho na vyakula vya Mifugo

Kuhamasisha wafugaji juu ya matumizi ya mabaki ya mazao na vyakula vingine

Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ufugaji wa kibashara

Kuelimisha wafugaji juu ya uvunaji wa mifugo na kuanzisha miradi mingine ambayo itawaongezea kipato

Kusimamia sheria ya nyanda za malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo

2.0 TAKWIMU ZA MIFUGO

AINA YA MIFUGO	IDADI YA MIFUGO
Ng'ombe	7,030
Ng'ombe wa maziwa	1,028
Mbuzi	2,309
Kondoo	2,108
Kuku	24,215
Nguruwe	7,087
Bata	768
Sungura	124
Kanga	103
Punda	4
Mbwaa	3561
Paka	982

Chanzo: Idara ya mifugo , Disemba 2016

3.0 MIUNDO MBINU YA MIFUGO

Idadi ya miundo mbinu katika Halmashauri ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatato hapa chini.:-

S/N	MIUNDOMBINU	ILIOPO	INAYOFANYA KAZI	MBOVU
1	Machinjio	1	Iko hatua ya mwi-sho ya ujenzi	0
2	Machinjio ndogo (Slaughter slabs)	2	2	0
3	Maduka ya kuuzia nyama	64	62	2

4.0 WASAMBAZAJI WA PEMBEJEZO ZA MIFUGO

NA	JINA LA DUKA	ENEOLILIGO
1	Divine Agrovet	Ifakara Mjini
2	Divine Agrovet	Kibaoni
3	Ephraimu Agrovet	Ifakara Mjini
4	Malugu Agrovet	Ifakara Mjini

1.3. SEKTA YA UVUVI

1.3.1.SERA YA UVUVI

Sera ya Uvuvi inasitizira Kusimamia uhifadhi, na usimamizi endelevu wa rasilimali za Uvuvi kwa manufa ya kizazi cha sasa na kinachokuja. Shughuli ya uvuvi inachangia takribani 25% ya kipato cha wakazi wa Ifakara.Pamoja na ajira na kipato faida zingine za Uvuvi ni kuongeza uhakika wa chakula na lishe katika Jamii.

1.3.2. MAJUKUMU YA SEKTA.

Majukumu ya Sekta ya Uvuvi ni pamoja na;

Kusimamia matumizi na utekelezaji wa Sera ya Uvuvi (1987),Sheria ya Uvuvi Na.22 (2003) na Kanuni za Uvuvi (2007).

Kushauri matumizi ya zana na teknolojia za kisasa za Uvuvi endelevu.

Kuhamasisha Ufugaji wa Samaki ili kupunguza utegemezi kwenye maji ya asili na kongeza kipato cha kaya.

Kudhibiti uvuvi haramu kwenye mito na mabwawa ya asili.

Kukusanya mapato ya Serikali

Kukusanya na kuandaa takwimu za uvuvi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Kuhakiki usafi na ubora wa samaki.

Kuboresha mazao ya samaki,matumizi na uhakika wa masoko

Kuandaa taarifa za kazi za kitengo za mwezi, robo na mwaka.

1.3.3.RASILIMALI ZA UVUVI

Shughuli za uvuvi zinafanyika kwenye Mito na Mabwawa ya asili, pia kuna shughuli za Ufugaji wa Samaki ambazo zinafanyika kwenye mabwawa ya kuchimba.



MITO

Ndani ya eneo la Halmashauri ya Mji Ifakara kuna jumla ya Mito ya Kudumu 2 na mito ya msimu 6. Mito hii ya msimu baadhi ilikuwa inatirirsha maji mwaka mzima lakini kutokana na uharibifu unaofanywa na shughuli za kibinadamu pamoja na mabadiliko ya tabianchi sasa inakuwa na maji kipindi cha Masika tu.

Jedwali : Mito ya kudumu na msimu.

NA	KATA	MITO YA KUDUMU	MITO YA MSIMU
1.	Ifakara	Kilombero	-
2.	Lumemo	Lumemo	Doko
			Kihogosi
3.	Kibaoni		Lungongole
			Kikwawila
			Kilama
			Matawale
	JUMLA	2	6

Chanzo; Idara ya Mifugo na Uvuvi Machi, 2017.

MABWAWA

Kuna jumla ya Mabwawa 89 kati ya hayo 52 ni mabwawa ya asili na 37 ni mabwawa ya kuchimbwa yanayohusika na ufugaji na uzalishaji wa samaki.

Jedwali :. Rasilimali za Uvuvi ndani ya Halmashauri ya Mji Ifakara.

Idadi ya Wavuvi	Mitumbwi	Boti	Mialo
264	52	4	6

MADUKA YA KUUZIA SAMAKI- Yapo maduka manne (4) ya kuuzia samaki



AINA YA SAMAKI

Zipo aina ya samaki zipatazo ishirini zinazopatikana kwenye mito na mabwawa hayo ya asili, zikiwemo aina mbili za samaki ambazo zinapaa Kilombero pekee ambazo ni Mbala na Mgundu. Kwa upande wa ufugaji samaki, zipo aina mbili ya samaki wanaofugwa ambao ni Sato (Kambale).

AINA ZA UVUVI

Ziko aina tatu za mbinu za uvuvi zinazotumika, ambazo ni pamoja na;

- ◆ Nyavu
- ◆ Ndoano
- ◆ Mitego

UCHAKATAJI WA SAMAKI

Ziko aina kuu tatu za teknolojia ya uchakataji wa samaki;

- ◆ Kubanika kwa kutumia moshi
- ◆ Kukaanga
- ◆ Kugandisha/barafu

UZALISHAJI WA SAMAKI

Halmashauri ya Mji Ifakara kuptitia maeneo yake ya Uvuvi, masoko na magenge imekuwa ikinakili samaki wanaovuliwa na kuuzwa kwenye Halmashauri. Wapo samaki wanaovuliwa ndani ya eneo na nje ya eneo la mji na wapo ambao husafirishwa nje ya Halmashauri. Uzalishaji kwa mwaka huwa unapanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali kwa kutegemea hali ya hewa na mabadiliko na tabianchi, nk.



Mto Kilombero ambao ni chanzo kikuu cha Uvuvi wa Samaki katika Mji wa Ifakara

UFUGAJI WA SAMAKI

Ufugaji wa samaki ni teknolojia muhimu sana katika kuboresha lishe, ajira, kuongeza kipato, kuhakikisha uwepo na usalama wa chakula. Halmashauri ya Mji Ifakara inayo maeneo yenye fursa za uwekezaji kwa ajili ya kufuga samaki kama inavyooneshwaa kwenye majedwali hapo chini.

Jedwali : Idadi ya Mabwawa ya kufugia samaki na maeneo yaliyopo



Bwawa Darasa la kufugia Samaki lilitopo katika Uwanja wa Halmashauri ya Mji Ifakara kwa ajili ya Maonesho ya Kilimo na Mifugo NaneNane Mkoani Morogoro

MAFANIKIO YA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI



Mkuu wa Wilaya ya Kilombero Mh.James Ihunyo akishiriki kutoa elimu ya Upigaji Chapa Mifugo katika Kata ya Michenga

Idara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kutoa ajira kwa Wafugaji, Wavuvi, Wafanyabiashara wa samaki/nyama, nk. Hata hivyo ufügaji unaendelea kuchangia katika kukuza kipato cha kaya na kuongeza lishe katika jamii. Idara imeweka malengo ya kuongeza kasi ya uhamasishaji wa kufuga mifugo/samaki katika maeneo yote yenyе sifa za ufügaji .

Mafanikio ni pamoja na:

- Kutoa elimu ya Ufugaji Mifugo/samaki kwenye Kataa 9 zilizopo katika Halmashauri.
- Kuanzisha vikundi 4 vya Ufugaji Samaki
- Kufanikiwa kufanya Utambuzi na usajili wa mifugo yote
- Kudhibiti uvuvi haramu kwa kukamata kokoro/ vyandarua na kuziteketeza.
- Kushirikisha jamii kupiga vita uvuvi haramu.
- Kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Kuzalisha na Kufuga Samaki pamoja na kuanzisha shamba darasa la kuku

Kuendelea kujenga miundo mbinu ya mifugo kama vile machinjio na makaro ya kuchinjia mifugo



Wafugaji katika Mji wa Ifakara wakionesha kadi zao mara baada ya zoezi la kutambuliwa, kusajiliwa na kupigwa chapa ifugo yao



Afisa Mifugo Bibi Juliana Mmasi akitoa Maelezo kwa Wanafunzi wa Mifugo